



TRC imeongeza Huduma ya Usafiri wa Abiria kwa treni ya Deluxe mara mbili kwa wiki kutoka Dar es Salaam (Alhamis Saa 2 Asubuhi na Jumapili Saa 4 Asubuhi) na kutoka Kigoma (Ijumaa saa 2 Usiku na Jumatatu Saa 2 Usiku)

TRC YAENDELEA KUWA KARIBU NA WADAU KWA KUWALIPA FIDIA WALIOPITIWA NA MRADI WA SGR



Maafisa kutoka Shirika la Reli Tanzania - TRC wakishirikiana na Viongozi wa Mtaa wa Gongo la Mboto uliopo Kata ya Gongo la Mboto na mtaa wa Mwembeni uliopo Kata ya Ukonga katika zoezi la Ulipaji fidia ya Makaburi yaliyohamishwa ili kupisha Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR hivi karibuni 2018.



Mkurugenzi Mkoo wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kadogosa (wa tatu kulia) akizungumza wakati wa kikao kujadili namna ya kusaidia maendeleo ya Elimu wilaya Kisarawe kilichofanyika katika Ofisi ya Mkoo wa Wilaya ya Kisarawe hivi karibuni 2018.




Mkurugenzi Mkoo wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kadogosa (wa tatu kushoto), Mkoo wa Wilaya ya Kisarawe Mhe. Jokate Mwegelo (wa tatu kulia) wakiwa katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa TRC na wawakilishi wa Kampuni ya Yapi Merkezi hivi karibuni 2018.



Kaimu Meneja Uhusiano wa Shirika la Reli Tanzania Jamila Mbarouk (kulia) kwa niaba ya Mkurugenzi Mkoo akikabidhi Mclele gunia 15, Maherage gunia 5, Mafuta ya kupikia ndoo 5 na karatasi za kusomea kwa Afisa Elimu Wilaya ya Kisarawe Bi. Jeneroza Nyoni kutimiza ahadi ya Mkurugenzi Mkoo wa TRC Masanja Kadogosa kusaidia Maendeleo ya Elimu Kisarawe kwa kujenga Madarasa na kutoa Chakula kwa Wanafunzi walio kambini kwa ajili ya kujiandaa na mitihani, hivi karibuni 2018.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe (kulia) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkoo wa TRC Masanja Kadogosa (wa pili kulia) kuhusu Maendeleeo ya Ujenzi wa Daraja la treni ya umeme linalojengwa Dar es Salaam hivi karibuni 2018.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe (wa nne kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkoo wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa (wa tatu kushoto) alipotembelea karakana ya Reli jijini Dar es Salaam hivi karibuni 2018.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe (aliyesimama) akizungumza na wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania - TRC (hawapo pichani) alipotembelea Ofisi ya makao makuu Shirika la Reli Tanzania Dar es Salaam hivi karibuni 2018.



Wafanyakazi wa TRC wakifuatilia hotuba kutoka kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwelwe wakati wa ziara Ofisi ya makao makuu Shirika la Reli Tanzania Dar es Salaam, karakana ya reli na kambi ya SGR iliyopo Ilala hivi karibuni 2018.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kadogosa (kushoto) akimueleza Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Humphrey Polepole (kulia) maendeleo ya Ujenzi wa Reli ya Kisasa wakati wa ziara kuona maendeleo ya ujenzi wa SGR nje kidogo ya kambi ya Soga Kibaha mkoani Pwani hivi karibuni 2018.



Meneja Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Maizo Mgedzi akiwaeleza, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Humphrey Polepole, Mwenyekiti wa Bodii ya Wakurugenzi ya TRC Prof. John Kondoro, Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa na Mwenyekiti wa CCM mkoaa wa Dar es Salaam Bi. Kate Kamba kuhusu maendeleo ya Ujenzi wa Daraja la treni ya Umeme linalojengwa kuanzia Dar es Salaam Stesheni ya Dar es Salaam hadi Ilala hivi karibuni 2018.

Mhandisi kutoka kampuni ya Yapi Merkezi akiwaeleza Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Humphrey Polepole, Mwenyekiti wa Bodii ya Wakurugenzi ya TRC Prof. John Kondoro, Mkurugenzi Mkuu wa TRC ndugu Masanja Kadogosa na Mwenyekiti wa CCM mkoaa wa Dar es Salaam Bi. Kate Kamba kuhusu hatua za ujenzi wa daraja la treni ya umeme linalojengwa kuanzia Dar es Salaam Stesheni hadi Ilala hivi karibuni 2018.